

ILIMPASA KUPITIA NJIA HII



Hebu tuendelee tu kusimama kwa muda mfupi tunaposoma Neno la Mungu. Nilikuwa nikiwazia juu ya utambulisho huo wote, hakika ingenibidi kuishi maisha halisi kutimiza hayo, sivyo? Huyu ni mtu anayekupenda. Katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 19, ninataka tu kusoma sehemu ya Maandiko, vifungu vitano vya kwanza.

Naye Yesu alipoingia Yeriko alipita katikati yake.

Na tazama, palikuwa na mtu, jina lake Zakayo, aliyekuwa na . . . mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye ni tajiri.

Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, maana ni mfupi wa kimo.

Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kuipitia njia ile.

Na Yesu, alipofika mahali pale, alitazama juu, akamwona, akamwambia, Zakayo, shuka upesi, . . . kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.

Akafanya haraka, akashuka, akamkaribisha kwa furaha.

Hata watu walipoona, . . . walinung'unika wote, wakisema, Ameingia kukaa kwa mtu mwenye dhambi.

Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne.

Yesu akamwambia, Leo wokovu umefika nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Ibrahimu.

Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.

Na tuombe.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa sababu Wewe ungali unatafuta kuwaokoa wana wa Ibrahimu, wale waliopotea. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utapokea ombi letu nyenyekevu na kubariki kukusanyika kwetu hapa leo hii. Na jalia kusiwe ni bure, bali jalia Roho Mtakatifu mkuu atufundishe njia ya Uzima, tukifahamu hili, kwamba hatuna budi kusimama katika Uwepo Wake siku moja, kutoa hesabu ya yale tuliyofanya na maisha haya. Tubariki pamoja sasa tunapoendelea kukungojea. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

³ Hakika nina furaha kuwa na marafiki wema, watu wanaoamini, na kuamini juhudi unazojaribu kuweka. Iwapo ningekuwa na madhumuni yoyote mengine, ili tu kuwa tofauti, mbona, ningekuwa mwenye dhambi ha—halisi. Lakini madhumuni yangu ni kumtukuza Yesu Kristo.

⁴ Na kitu fulani kilicho ndani ya mwanadamu, unapokuwa na Ujumbe kutoka kwa Mungu, huwezi kujizuia. Kuna kitu ndani yako, kinadundadunda. Kinaendelea, kwa vyovyote vile. Huwezi kukipoza, kukikomesha, au kukianzisha. Kinakoma na kuanza na kukutuliza. Unaona? Ndicho kilicho na udhibiti.

⁵ Shukrani kwa—kwa ndugu hawa wema kwa ushuhuda wao wa Bwana wetu Yesu. Hawakuwa wakinena habari zangu, bila shaka sivyo. Walikuwa wakinena habari Zake.

⁶ Kama nilivyokuwa nikisoma makala mafupi, hapa si muda mrefu uliopita, kuhusu Bw. Moody. Kasema, Chicago ilikuwa inaenda kuninii. . . gazeti lilikuwa linaenda kuandika maelezo ya mhariri juu yake. Basi wakamtuma mtu, akatafute kujua ni kwa nini watu walikusanyika kumsikiliza Bw. Moody. Maelezo ya mhariri; Bw. Moody ni kama mimi, hakuwa na elimu ya kutosha kusoma ma—maelezo ya mhariri, kwa hiyo ilibidi meneja wake kuyasoma. Bw. Moody alikuwa ni mshona viatu, hapo awali, ndipo akaitwa na Mungu kwa ajili ya ujumbe wa—wa wakati huo. Basi kwa hiyo meneja alikuwa akiyasoma maelezo ya mhariri, nayo yalisema, “Ni kwa nini mtu aende kumsikiliza Dwight Moody?” Kasema, “Kitu cha kwanza, ndiye mtu mwenye sura mbaya kuliko wote niliopata kuona.” Pia kasema, “Ana upara kichwani, na sharafa ndefu, na kadhalika.” Tena kasema, “Na yeye—yeye hutoa sauti kama ya mlio wa farasi anapongea. Sarufi yake ndiyo mbaya kuliko zote nilizowahi kusikia.” A-ha. Na, loo, alikuwa tu akiendelea namna hivyo.

⁷ Kasema, “Bw. Moody akainua tu mabega yake. Akasema, ‘Hakika sivyo. Wao huja kumwona Kristo.’”

⁸ Kwa hiyo, hilo ni, nafikiri hilo tu ndilo jibu. Ni Kristo ndiye tunataka kumwona. “Nikiinuliwa juu, nitavuta watu wote Kwangu.”

⁹ Nilikuwa nikiwazia, baada ya kuzuru hapa katika ji—jiji, na kuona ya kwamba watu, jinsi ambavyo wamekuwa wema, mkutano mzuri sana tulio nao hapa katika Denham Springs High School, au ukumbi wa shule. Nilikuwa nikiwazia, watu hapa ni kitu kama kahawa. Wao ni. . . Jamani! Si wingi, bali ni ubora; kiasi kikubwa katika kimoja cha vikombe hivyo.

¹⁰ Ninakumbuka mara yangu ya kwanza nikitua kwenye uwanja wa ndege hapa nje. Ndugu wakija kunichukua, nimeketi hapa. Ndipo msichana mdogo wa Kifaransa pale; nikamwomba hambaga na kikombe cha kahawa.

¹¹ Sikuwahi kuinywa mpaka nilipokuwa na yapata umri wa miaka thelathini na minane; nilipaswa kujua bora zaidi. Lakini hata hivyo Ndugu Brown, nadhani yupo hapa asubuhi ya leo, mahali fulani. Ameketi moja kwa moja hapa. Alipendezwa nayo sana, naye akanipa. . . Ngingekuwa na kiamshakinywa cha huduma saa moja, nyingine saa mbili, na nyingine saa tatu; usingeweza kula hivyo vyote, kwa hiyo wangemimina kahawa. Nami nikaanza kuionja kidogokidogo, na, muda si muda, nikawa ninainywa.

¹² Basi nikamwuliza msichana huyu, nikamwambia, “Ninataka hambaga na kikombe cha kahawa.” Walipokileta hicho kikombe kidogo, nikawaza, “Jamani, jamani, ni wachoyo kweli kwa kahawa yao hapa.” Mkupuo wa kwanza, kumeza kwa kwanza nilikofanya, loo, jamani, nilipata shida kupumua. Mnaona?

¹³ Maskini msichana huyo akasema, “Hapana shaka wewe ni Yankee.” Akasema, “Nitakutengenezea kikombe cha Yankee.”

¹⁴ Kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyowaona watu, labda si umati mkubwa kuliko wote niliowahi kuzungumzia, bali ubora halisi wa kweli. Ninashukuru kwa hilo, kusanyiko linalosikiliza, mtu anayeketi na kusikiliza yale unayosema. Mimi. . .

¹⁵ Hayo ndiyo ninataka ufanye. Kuchunguza yale anayosema mtu, kwa Neno la Mungu. Ndipo, kama si sahihi, basi si sahihi. Ni hivyo tu. Ikiwa ni Neno la Mungu, basi Mungu hana budi kulitetea Neno Lake, maana aliahidi kufanya hivyo. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyopenda kuchunguza mambo haya, ku—kuona.

¹⁶ Sasa nimeelewa, asubuhi ya leo, kwamba hiki kilikuwa kiwe kiamshakinywa cha wafanyabiashara, na Wafanyabiashara wa Full Gospel, ambao mimi ni mwanachama wa tawi lao. Nami nafikiri hiki. . . Walisema baadhi yao walikuwa hapa. Baadhi yao hawakuondoka. Labda, ni wafanyabiashara, wana biashara yao hawana budi kuishughulikia. Nitawapa udhuru, kwa vyovyote vile, kwa hiyo—kwa hiyo hiyo ni sawa. Alisema wengi wa watu wao walikuwa hapa, hata hivyo, kwa hiyo hilo ni jema sana.

¹⁷ Sasa utani mdogo tu. Nimeutaja, lakini labda. . . Si mahali pa kufanya utani, bila shaka, bali ni ucheshi kidogo tu. Unapozungumza, kama vile tumekuwa tukifanya, muda mfupi uliopita, vema, labda urudishe watu kwenye ucheshi mdogo.

¹⁸ Ninakumbuka wakati mmoja, mimi na rafiki yangu tulikuwa shuleni pamoja. Jina lake lilikuwa Wilmer Snyder. Ndugu yake ni mhudumu wa Kibaptisti, na yeye—yeye huandika kwenye hili *Chumba Cha Juu*, ma—makala maalum katika *Chumba Cha Juu*. Tulikuwa wavulana wa shule pamoja. Nami nilijifunza huduma, na yeye—yeye akawa wakala wa bima. Ndipo basi akaja nyumbani kwangu, siku moja, kunitembelea. Na sasa huenda

kuna baadhi ya mawakala wa bima hapa. Nami sisemi chochote juu ya bima sasa. Natumai, msiwazie mabaya juu ya hili, bali mpate ufahamu mdogo wa kile mimi . . . jinsi nilivyolisema. Kwa hiyo ndugu yangu pia ni—yuko na Prudential, naye anauza bima ya Prudential.

¹⁹ Kwa hiyo wakati mmoja nilikuwa na kitu kidogo kimefanywa na kampuni ya bima ambacho nina . . . nadhani, pasipo kujua sana, mimi . . . walinisomea hati ya bima vibaya, nami nikaelezewa visivyo, na mimi sikugundua hilo. Mimi . . .

²⁰ Kwa hiyo, siku moja, Wilmer alikuja kuniona, naye akasema, akasema, “Unaendeleaje, Billy?”

Nikasema, “Vema.”

Kasema, “Ninasikia umekuwa huko nje mikutanoni!”

Nikasema, “Naam, niko nje mikutanoni.”

²¹ Nilikuwa nikimwambia kuhusu jamaa aliyeniambia. Akasema, “Aisee, wewe ni mhubiri. Unafanya nini, kurandaranda karibu na hawa wafanyabiashara?”

Nikasema, “Mimi ni mfanyabiashara.”

Nao wakasema, “Aa, unafanya biashara gani?”

Nikasema, “Biashara ya dhamana.”

²² Na, unaona, hakuelewa hilo. Sikusema, “Bima.” Nilisema, “Dhamana.” Unaona?

Basi kwa hiyo nikasema, “Biashara ya dhamana.”

²³ Akasema, “Loo,” kasema, “Naelewa.” Akasema, “U—unauza bima gani?”

²⁴ Nikasema, “Ninauza dhamana ya Uzima wa Milele.” Na ningali ninaiuza. Kwa hiyo ningefura— . . . yeyote wenu atakaye, ningependa kuijadili hati hiyo na wewe, moja kwa moja baada ya mkutano, ikiwa ni sawa.

²⁵ Kwa hiyo basi akasema, akasema, “Uzima wa Milele?” Kasema, “Siamini nimewahi kusikia kuhusu kampuni hiyo.”

²⁶ Nikasema, “Loo, hujawahi kusikia?” Nikasema, “Inajulikana sana.” Ndipo akasema . . . Nikasema, “Ni kampuni ya kale.”

Naye akasema, akasema, “Yako wapi makao makuu?”

Nikasema, “Utukufuni.”

²⁷ Wilmer akaniambia, kasema, “Billy, niliwazia ningekuja, nikuuzie bima fulani.” Kasema, “Nasikia kwamba huna bima yoyote.”

Ndipo nikasema, “Loo, naam. Ni—niko na dhamana.”

²⁸ Naye akasema, “Loo, samahani.” Akasema, “Nadhani, ndugu yako, alikuuzia.”

Nikasema, “La, si na yeye hasa.”

29 Mke wangu akaniangalia, kana kwamba alitaka kusema, “Vema, bila shaka unasimulia hadithi.” Alijua sikuwa na bima yoyote. Lakini hata yeye pia hakuelewa. Nilisema, “Dhamana,” sio “bima.”

Akasema, “Una bima gani, Billy?”

30 Nikasema:

Dhamana yenye Baraka, Yesu ni wangu!
Loo, ni kionjo cha jinsi gani cha utukufu wa
Kiungu.
Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na
Mungu,
Nimezawa kwa Roho Wake, nikaoshwa kwa
Damu Yake.

31 Akasema, “Billy, hiyo ni nzuri sana. Hiyo ni nzuri sana.” Kasema, “Sina chochote dhidi ya Hiyo, lakini,” kasema, “Hiyo haitakuweka huko juu hapa kaburini wakati ukiondoka.”

32 Nikasema, “Itanitoa huko. Sina wasiwasi kuhusu kuingia.”

33 Sina wasiwasi kuhusu kuingia; ni, kutoka. Na kwa hiyo—kwa hiyo *Hii* ndiyo kitu pekee nijuacho kitakachokutoa. Kwa hiyo ikiwa ungetaka kutoka, hebu tuzungumze nawe kuhusu Hiyo.

34 Nikiwatazama wasikilizaji, asubuhi ya leo, sitawaweka ila kidogo tu. Nami nilikuwa na fungu nililokuwa ninaenda kuhubiria, kwa hiyo basi nikawaza, vema, afadhali nisifanye hivyo. Nilikuwa tu naenda kuwa na mchezo mdogo wa kuigiza juu ya jambo fulani, mtu fulani katika Biblia.

35 Ninawazia hapa kuhusu mambo mazito. Kwamba, wakati tunapoketi hapa kama Wakristo, nadhani wengi wetu, hivi unajua huu huenda ukawa ndio wakati wa mwisho tutakaopata kula kiamshakinywa pamoja? Je! uliwahi kufikiria kuhusu hilo?

36 Hivi unatambua, maneno madogo yanayonipasa kusema hapa, Mungu atanifanya kujibu kwa hayo huko juu kwenye Siku ya Hukumu? Unaona? Nami ninazo nafsi hapa, haidhuru kama ni kundi dogo, bali hata hivyo inanibidi. Ni maneno ninayosema, vema, itanibidi kujibu kwa ajili ya hayo Huko juu.

37 Kwa hiyo huenda tusile kiamshakinywa kingine pamoja, bali natumaini tutakula Chakula cha jioni pamoja, siku moja. Hicho ni chakula cha jioni cha mwisho, Huko juu pamoja na Yeye, kitakuwa ndicho cha kwanza Huko.

38 Na basi tunapoketi hapa asubuhi ya leo, nami ninawaangalia watu hawa hapa, baadhi yao, wahudumu mashuhuri ambao wameelimika. Na mimi, hapa, m—mtu wa msituni tu aliyejitokeza, bila elimu, nikiketi hapa na watu waliohitimu kuhubiri, na Madaktari wa Uungu. Ninajisikia duni sana kusimama na kuzungumza mbele ya watu kama hao. Lakini, hata hivyo, si—sina budi kueleza yale ninayojisikia. Na shukrani

zao kuu na ukarimu kuniruhusu nisimame na kufanya hili. Ninathamini hilo, ndugu zangu, kushirikiana katika mkutano, na kuja pamoja. Nipo hapa kuwasaidia. Nitafanya kila niwezacho kwa kila mmoja wenu, kwa neema ya Mungu.

³⁹ Ndipo basi yote yakiisha, siku moja, nisipoweza kula kiamshakinywa pamoja nanyi tena, yote yakiisha, tunaketi upande mwingine wa meza mmoja na mwenzake, huo ndio wakati ambao ninatazamia. Hapana shaka ila machozi machache yatatiririka mashavuni mwetu, na kuangalia upande wa pili wa meza na kushikana mkono mmoja na mwenzake. Itamaanisha kitu wakati huo. Hebu tufanye kazi ukiwa ni wakati wa kufanya kazi, wakati jua likiwa juu. Litatua baada ya kitambo; linateremka chini kabisa. Halafu, kuwazia kwamba, wakati tukiketi pale, tumeshikana mikono, na kulia kidogo, ndipo Mfalme mkuu atajitokeza, amevaa mavazi Yake yote makuu, ashuke kwenye safu, apanguse machozi yote kutoka machoni mwetu, na kusema, “Mmefanya vyema, watumishi wangu wema na waaminifu, ingieni katika raha za Bwana, mlizoandaliwa tangu misingi ya ulimwengu.” Wakati jua likiwa juu, na kuna mwanga wa kutosha kufanya kazi, hebu tufanye kazi.

⁴⁰ Sasa fungu hili dogo hapa, huenda likaonekana la kuchekesha, bali tutazungumzia somo hili: *Ilimpasa Kupitia Njia Hii*.

⁴¹ Hapana shaka ulikuwa usiku wa—wa kutisha kwa maskini jamaa huyu. Asingeweza kulala hata kidogo, naye aligeukageuka tu na kugaagaa, usiku kucha. Kulikuwa kunapambazuka.

⁴² Nasi sote tunafahamu kinachomaanisha kuwa na usiku wenye usumbufu, huwezi kulala. Unalo jambo fulani moyoni mwako, ama kitu fulani kinakufadhaisha.

⁴³ Naye maskini jamaa huyu alikuwa ni mfanyabiashara, labda katika mji wa Yeriko, ambacho kilikuwa kitu kama ninyi wanaume na wanawake wafanyabiashara hapa, na yeye—yeye bila shaka alikuwa na biashara iliyokuwa ikipanuka. Alikuwa na sifa sana na... vilabu vyote, na kadhalika, na alikuwa mshiriki wa kanisa, baraza la Sanhedrin, na walikuwa na kuhani mzuri, na alimwamini kuhani huyu.

⁴⁴ Na jambo la ajabu kuhusu kisa hiki, hata hivyo, ni mke wake. Tutamwita Rebeka. “Alikuwa amepotoka akaenda upande usiofaa,” aliwazia, vivyo hivyo na kuhani. Alikuwa anamfuata Mtu aliyedhaniwa kuwa nabii wa Nazareti, Mtu jina lake Yesu. Watu, tabaka la watu maskini, walimwamini kuwa nabii, au Masihi aliyeahidiwa, bali haikutimiza kabisa masharti ya Sanhedrin.

⁴⁵ Ajabu, wakati mwingine Mungu hufanya mambo kinyume na vile tunavyofikiria. “Jamaa huyu, mnaona, alizaliwa,” kwa

maoni yao, “kuzaliwa kiharamu. Mama yake alimzaa kabla ya yeye na mume wake kufunga ndoa.”

⁴⁶ Jambo lingine, Yeye hakuwa na elimu. Hawakuwa na rekodi yoyote Yake kuwahi kwenda shule. Hakuwa kuhani, wala hakuwa rabi. Alikuwa tu na madai, kama, Yake Mwenyewe.

⁴⁷ Kama vile Ndugu Don alivyotaja kiutukufu asubuhi ya leo, “Ilikuwa ni kupiga kona.” Hawakuitambua. Daima hufanyika hivyo. Ilifikia wakati huo wa kupiga kona.

⁴⁸ Lakini kwa njia moja, au nyingine, mke wake alikuwa ameshawishika kwamba Huyu alikuwa ndiye yule Nabii aliyekuwa aje, na alikuwa amemfuata, akamwamini.

⁴⁹ Naye alikuwa amejaribu kumwambia mumewe. Lakini alikuwa amechukuliwa sana katika biashara yake, na pamoja na... Alikuwa ni mshiriki wa kanisa. “Hiyo si ni nzuri vya kutosha?”

⁵⁰ Kitu kama yule kijana mtawala tajiri, mwajua. Alikuwa na biashara, pia. Lakini alitambua kwamba alikuwa m—mfuasi wa kanisa, bali hakuwa na Uzima wa Milele. Ndipo akauliza... Aliona kitu fulani ndani ya Yesu ambacho watu wengine hawakuwa nacho. Basi akasema, alimjia na kusema, “Mimi...” Alitaka kujua kama yeye... kile ambacho angeweza kufanya ili kuwa na Uzima wa Milele. Naye Yesu akamwambia azitii amri. Akasema, “Nimefanya haya tangu nilipokuwa kijana.” Mnaona, ilionyesha alikuwa m—mwaminio, bali alijua kwamba Yesu alikuwa na kitu ambacho hao makuhani na rabi hawakuwa nacho.

⁵¹ Na mtu akikutana na Yesu Kristo, Yeye ni tofauti na wanadamu. Wewe si yule yule unapomwona mara moja, iwapo kuna kipengee chochote cha Mungu kwako.

⁵² Kwa hiyo Rebeka alikuwa amempata huyu Yesu. Na Yeye—Yeye alikuwa, kwake, timizo hasa la ahadi ambayo Wayahudi walikuwa wakitazamia, kwa ajili ya siku yao.

⁵³ Kwa hiyo habari zilikuwa zimeenea kwamba Yeye alikuwa awe na kiamshakinywa, ama namna fulani ya chakula cha kutwa au kitu kama hicho, huko chini Yeriko, kwa hiyo alikuwa ameshughulika kuomba kwa ajili ya mume wake mfanyabiashara.

⁵⁴ Tunahitaji Rebeka wengine, kila mahali, mnaona. Mnaona, maombi hubadilisha mambo. Ukimweka mume wako, ama jamaa yako asiyeokoka, mbele za Mungu, na kisha uombe, Mungu atafanya njia mahali fulani, maana aliahidi kufanya hivyo.

⁵⁵ Basi hiyo ndiyo Rebeka, akiwa ni mwaminio thabiti na mfuasi wa Bwana Yesu, na hapana shaka alikuwa mtu mwema sana, na alikuwa... anaijali nyumba yake.

56 Nami nafikiri hiyo inaonyesha tena, kwamba ikiwa—ikiwa mtu akikutana na Yesu na kuwa Naye kwa hakika moyoni mwako, unajali sio tu nyumba yako mwenyewe, bali nyumba ya Mungu, kila mahali. Unajali, kwamba wamjue Yeye. “Na kumjua Yeye ni Uzima.” “Kumjua Yeye,” unaona, sio kujua jinsi ya kusoma Neno, ama kitu kama hicho. Bali, “Kumjua Yeye, ni Uzima.”

57 Kwa hiyo alikuwa ameomba kwa bidii. Na siku ikakaribia ambapo Yesu alipaswa kuingia mjini. Na hapana shaka ila, siku moja kabla, huenda aliona kama fikra zake zimebadilika angalau. Kwa hiyo akasema, labda, “Zakayo, u—unaenda kwenye kile kiamshakinywa asubuhi?”

58 “Mbona, bila shaka siendi. Mbona, lile kundi la watu! Nawe unanitarajia. . . Ninao mkahawa mzuri kuliko yote mjini, halafu wanakiandaa kwa Lavinski.” Natumai hakuna Lavinski hapa. Lakini, hata hivyo, “Huko mahali kwingine, unaona. Na, mbona, nina mahali pazuri kuliko pote mjini, nao wakachagua mahali pale huko chini. Mbona, hawakupaswa kufanya hivyo. Walipaswa kuja mahali pangu, kuandaa hiki, waona.” Alikuwa haendi.

59 Ndipo akaanza kuomba, kwa shauku kubwa mno. Kwa hiyo basi usiku huo, maskini jamaa huyo asingetulia hata kidogo.

60 Mwajua, kuna jambo fulani kuhusu hilo, kama ukianza kuomba kwa shauku kubwa kuhusu jambo fulani, Mungu hufanya kazi pande zote mbili, unaona. Yeye—Yeye—Yeye hujibu.

61 Basi maskini jamaa huyo, hapana shaka alianza kufikiria usiku huo, “Sijui kama inafaa niende huko chini na—na—na kumsikia Mtu huyu? Sasa, Rebeka anasema ati Yeye ni nabii. Sasa, tunajua hatujawa na manabii wowote kwa mamia ya miaka. Nami nilimwuliza kuhani kuhusu hilo, akasema, ‘Hakuna kitu ila upuuzi tu! Kama kungekuwa na Nabii anayeinuka, si angekuja kupitia kwenye kanisa? Hivyo ndivyo ingempasa kuja. Angetujia sisi Mafarisayo, au Masadukayo, au kundi letu, la sivyo asingekuwa ni Nabii.’” Mnajua, fikira hiyo ingaliko. Kwa hiyo wanawazia haina budi kuja kwa njia hiyo, la sivyo si sahihi. Kwa hiyo wakasema, hapana shaka, ila, katika wakati huu mkuu ambapo. . . Yeye aliliamini, hata hivyo.

62 Naye alikuwa amejadili hilo na kuhani. Kuhani akasema, “Sasa angalia hapa, siku za manabii zimekuwa miaka mingi, mingi iliyopita. Tunayo torati. Tunayo yote imeandikwa. Hali hii iko chini ya udhibiti, nasi tunaishughulikia, na tunajua kuhusu mambo haya.”

63 Lakini basi, bila shaka, Zakayo, bila kuangalia Hilo, akidhania tu kabisa, akilichukulia tu hivi hivi. Neno kudhania ni “kuthubutu bila mamlaka.” Mbona, a—alidhani kwamba hiyo

ilikuwa sawa; mradi tu alikuwa ni mshiriki wa kanisa, haya tu ndiyo yaliyompasa kufanya.

64 Lakini basi wakati usiku ulipoanza kuingia, kukaja shauku kubwa moyoni mwake. “Labda kama mtu huyu yuko mjini, huenda asirudi hapa tena. Yanipasa niende nichunguze ha—hali, nijionee mwenyewe.”

65 Sasa hilo ni wazo jema. Lichunguze wewe mwenyewe. Usiende kukosoa. Lichukue Neno, na ulichunguze Neno kwa hilo.

66 Kwa hiyo yeye, Rebeka, alikuwa amejaribu, kama mwanamke awezavyo, kueleza kile ambacho manabii walikuwa wamesema, na kile Musa alikuwa amesema, kuwa Mtu huyu angekuwa, na wakati anapokuja. Kwa hiyo hapana shaka aliwazia, akajaribu kumwelezea mume, lakini hata hivyo kuhani alikuwa na ushawishi mkubwa kwake kuliko jinsi Rebeka, mke wake, alivyokuwa nao.

67 Basi asubuhi ilipoanza kupambazuka, mbona, maskini jamaa huyo alikuwa... Rebeka, ninaweza kumwazia, nikimwona akimpigapiga, akisema, “Zakayo, wataka kuniambia kuwa hutaki kuenda huko chini?”

“La, sitaki uhusiano wowote na Hilo.”

68 Unajua, usiwe, Reb-... Usichukizwe, Rebeka. Wakati mwingine hiyo ni dalili nzuri. Unaona, wakati—wakati anaposhushwa moyo sana, wewe nena kuhusu Hilo, kila kitu kingine. Hiyo ni dalili nzuri kweli, wakati mwingine.

69 Kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, Rebeka anajifanya kuwa amelala. Ila, alikuwa akiomba. Naye anamwona Zakayo anatoka kitandani kisiri, kwa urahisi sana, wajua, kisha anaenda na kujinadhifisha vizuri, na kuchana nywele zake vizuri, na kuvaa vazi lake lililo zuri kuliko yote. Naye akachungulia, kutoka kwa jicho moja, kuona alichokuwa akifanya. Alijua papo hapo Mungu alikuwa amejibu maombi. Alijua jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia. Kwa hiyo Zakayo akatoka akinyatia kwa ncha za vidole, bila ya kumfanya Rebeka ajue anakoenda, mwajua. Naye anatoka kisiri, na anafika nje na kutazama nyuma.

70 Mke anainua pazia, anatazama nje, kumwona akitoka. Anasema, “Asante, Bwana. Yote ni sawa sasa hivi.” Mnaona?

71 Kama Eliya alivyofanya, wakati aliposema, “Ninaona hilo, wingu ukubwa wa mkono wa mwanadamu.” Dalili ndogo tu ya kwanza, kitu fulani kinakaribia kutendeka.

72 Kwa hiyo anatoka, na kuteremka mitaani. Akasema, “Sasa nasikia ataingilia lango la kusini, kwa hiyo afadhali niende pale na kusimama.” Tena kasema, “Nami nitajitafutia mahali, na nitasimama papo hapo. Ndipo anapoingia, nitaona kuwa jamaa huyo ni Nabii kiasi gani. Nami nitajitokeza moja kwa moja

na kutia kidole changu chini ya pua Yake, nami nitamweleza ukweli wa mambo, na wakati akija. Nami nitamwambia kwamba upuuzi Wake wote umemfanya mke wangu... na mikutano hii ya maombi na kadhalika. Ninachukizwa na kuchoshwa nayo. Nitamweleza. Nitasema jambo kuhusu hili, mnaona, nami nitamwambia. Na kisha ninajua rabi bila shaka atanipa pongezi, na kusema, ‘Zakayo, wewe ni mshiriki mwema wa kanisa hili hapa. Hakika wewe ni jamaa mwema.’” Kwa hiyo akasema, “Nitaenda huko chini mapema,” kwa hiyo akashuka.

⁷³ Alipokuwa yapata jengo moja, ama mawili, kufikia lango, akaona, hapo palikuwa pamejaa. Walikuwa wananing’inia kwenye kuta na kila mahali. Kwa njia moja ama nyingine, ingawa alinenwa habari Zake, kungali kulikuwa na mtu angalipenda kumsikia. Mtu fulani angesikiliza.

⁷⁴ Kwa hiyo akasema, “Sasa nitawezaje kumwona akiingilia langoni?” Kumbukeni, Biblia ilisema alikuwa mdogo wa kimo. Ndipo akasema, “Mimi ni mdogo sana.” Kwa hiyo akasukuma huku na huku, “Hapa, nipeni nafasi kidogo!” Unaweza kujua yeye si Mkristo bado, unaona, akitenda namna hiyo. Wakristo hawana mtazamo huo, mnaona. “Rudi nyuma! Unajua mimi ni nani? Mimi ni Zakayo. Mimi ndiye mwenye ule mkahawa hapa juu. Simile, toka njiani mwangu!” Mnaona? Sasa, huyo si Mkristo. Kila mtu alijua hakuwa. Labda baadhi yao walijua kwamba Rebeka alikuwa akiomba.

“Vema,” wakasema, “vema, wewe toka.”

⁷⁵ Na kwa hiyo alijua asingeweza kumwona kamwe, katika umati huo wote, hivyo asingeweza kumwambia fikira zake. Kwa hiyo akawaza, “Vema, sasa, nitafanya nini? Labda nitarudi nyumbani na kusahau tu jambo hilo.”

⁷⁶ Lakini, wajua, kuna jambo fulani kulihusu, kwamba ukiamua kuwa unataka kumwona, hakuna kitu kitakachokuzuia kumwona. Sijali ni kitu gani, una—unang’ang’ania, na kama vile yule maskini mwanamke Myunani alivyong’ang’ania aweze kumfikia Yesu. Na kuna jambo fulani kuhusu hilo, kwamba wakati wowote ukiamua kwamba unaenda kumwona, hakuna kitu kitakachokuzuia. Lakini, kumbuka, unapoamua, basi ibilisi atafanya kila kitu awezacho kukuzuia. Amekusudia kwamba hutalielewa, hutalionga. Atarusha kila pazia nyeusi mbele yako, awezalo, kukuzuia usilione.

⁷⁷ Kwa hiyo hicho hapo kizuizi chake cha kwanza, papo hapo. Kwa hiyo basi akaanza, kasema, “Vema, nadhani...”

⁷⁸ Kisha akaangalia kule, na hapo wamesimama baadhi ya washindani wake, na, wao, alijua hapo kwamba baadhi ya watu kutoka kanisani. Kwa hiyo hapo alikuwa amefanya mzaha mwingi sana kuhusu huyu Yesu wa Nazareti, kuhusu kuwa nabii, basi hapa wakasimama baadhi ya washiriki wake wakimtazama,

moja kwa moja pale katika kundi lile lile. Kamwe asingeweza kujificha. Alitambulikana.

⁷⁹ Sasa, Zakayo, tayari umetambulikana, kwa hiyo ninii tu...wajua, kama kulipata kuwa na mmoja hapa. Tayari umechangamana na kundi hili sasa, kwa hiyo tayari wanajua ni nani, tupo hapa, kwa hiyo afadhali tufahamiane, tujuane.

⁸⁰ Kwa hiyo akasema, “Vema, hii ni ajabu hapa.” Basi akaangalia kote, akamwona mmoja amesimama hapa. “Na unajua, hata hivyo, wote karibu ni kama wewe, wa—wanataka kuona kitu fulani.”

⁸¹ Mtu anajua kwamba alitoka mahali fulani, kutoka mbali sana; na akiondoka, anarudi mahali fulani. Naye daima anajaribu kutafuta kitu kujua mahali alikotoka na mahali anakoenda. Yupo Mmoja tu aliye na jibu hilo, huyo ni Mungu. Kila mtu anataka kuangalia kupita pazia hilo. Ndipo ukiona chochote ambacho... ambacho kinaweza kukuonyesha kilicho nyuma ya pazia hilo, mahali umekuwa, na kuwa wewe ni nani, na mahali unakoenda. Kipo Kitabu kimoja tu, kati ya vitabu vyote vilivyowahi kuandikwa, vya mamilioni ya tani, *Hiki* ndicho Kitabu kinachokuambia kuwa wewe ni nani, mahali ulikotoka, na mahali unakoelekea. Hakuna kitabu kingine kitakachofanya hilo; hiyo Biblia! “Nalo Neno ni Mungu,” Biblia ilisema.

⁸² Sasa, tunaona ya kwamba jamaa huyu, wote wakimzunguka, aliaibika kuona kwamba alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa wakipiga mayowe, na kulia, na kupiga makelele, na kutenda kama walikuwa wendawazimu. Kwa hiyo, lakini yeye... Huyo hapo ameketi, ametambulishwa nao, kwa hiyo i—ilimbidi tu kukaa, hakuna lingine. Sasa akasema, “Vema, ikiwa nimefika umbali huu, heri niendelee mpaka kweli nimwone.”

⁸³ Sasa, Zakayo, hilo ni wazo zuri. Tayari umefika hapa kwenye kiamshakinywa, kwa hiyo basi acha tuendelee tu. Mnaona, sote tumefika umbali huu.

⁸⁴ Kwa hiyo sasa tunaona, ya kwamba, walivyoziidi kuendelea, alisema, “Sasa nikikaa hapa, si—siwezi kumwona, maana mimi ni mdogo sana. Kwa hiyo, wajua, naamini nitaondoka kwenye umati huu, na nikimbilie kule kwenye kona ambapo nitasimama peke yangu, nijipatie mahali moja kwa moja ka—kando ya kijia. Na atakapokaribia, ndipo nitakapojitokeza moja kwa moja mtaani na kumwambia yale ninayowazia kumhusu. Nitamwambia ukweli wa mambo.”

⁸⁵ Basi akaondoka, mbali na umati huo, na kushuka chini. Akawaza, “Sasa Yeye atapitia njia gani?” Vema, akashuka akaenda kwenye “Barabara Kuu ya Haleluya.” Hiyo ndiyo njia ambayo Yeye hupitia daima, unaona. Kisha akaenda chini kwenye “Kona ya Amina,” mahali inapopiga kona, kuteremka kwenye—kwenye mahali pa kulia.

⁸⁶ Hapo ndipo unapoenda, wajua, “Barabara Kuu ya Haleluya” na “Kona ya Amina,” ndipo basi uko tayari kula Neno. Unaona? Unaona?

⁸⁷ Kwa hiyo akashuka akaenda kwenye kona hii, na kusimama hapo kwenye kona, kasema, “Sasa hakuna mtu hapa. Na wakati mimi...” Najua hili linasikika la kuchekesha, bali ninaninii tu... Shikilia kwa dakika moja. Kwa hiyo basi, muda si muda wajua, akafika kwenye kona hii, naye akasema, “Hakuna mtu hapa, kwa hiyo nitasimama hapa. Anapopitia, nitaona kuwa Yeye ni Nabii kiasi gani. Nitajitokeza moja kwa moja mtaani, nami nitamwambia jambo.”

⁸⁸ Kwa hiyo alikuwa amesimama pale, ndipo akaanza kuwaza, “Sasa kidogo tu. Unajua, kama nilikuwa mdogo sana huko chini, umati ule huenda utaenda popote anapoenda. Na mimi—mimi sitaki mtu yeyote anayepiga mayowe wakati ninapozungumza na Yeye. Ninataka nimwambie ili aweze kunisikia. Na hao wakipiga mayowe ‘Amina,’ na ‘Haleluya,’ na ‘Utukufu kwa Mungu,’ ‘Hosana kwa—kwa Nabii ajaye katika Jina la Bwana.’ Loo, kamwe hawatanisikia, kundi hilo lote lenye kelele. Kwa hiyo kuna jambo moja tu... Ndipo wote watanizunguka, na halafu si—si—siwezi hata kumwona hata kidogo.”

⁸⁹ Kwa hiyo ikawa kwamba alitazama, huku amesimama kwenye kona, na ulikuwapo na mti wa mkuyu wa kale uliojulikana pale. Huo ni mti mzuri wa Indiana. Basi amesimama kwenye kona. Akawaza, “Vema, kama ningeweza kupanda pale juu kwenye tawi lile halafu niketi, basi ningekuwa pale juu, halafu ningeweza kweli kumwambia wakati akipitia hapo.”

⁹⁰ Kwa hiyo akaja, akakimbilia pale. Naye alikuwa mdogo sana wa kimo; asingeweza kufikia tawi hilo. Kwa hiyo akasema, “Vema, sasa kuna jambo moja tu niwezalo kufanya,” na hapo palikuwepo ma—mapipa ya takataka ya mji, yamewekwa kwenye kona. Kwa hiyo akawaza, “Vema, sasa, kama nikienda na kuchukua hilo pipa la takataka, na kulinyanyua na kulileta hapa, basi ninaweza kufikia sehemu iliyobaki kuupanda mti huu kutoka kwa hilo. Hilo litanisaidia.”

⁹¹ Kwa hiyo anaenda pale. Na wazoa taka wa mji hawakuwa wamekuja, bado, asubuhi hiyo, nalo lilikuwa zito kwelikweli. Kwa hiyo yeye alikuwa mdogo na asingeweza kulinyanyua. Njia ya pekee ya kufanya hivyo, ilikuwa ni kulikumbatia kwa mikono yake. Naye alikuwa amevalia vazi lake lililo bora kuliko yote. Kwa hiyo, unajua, daima kuna vizuizi unapojaribu kumwona Yesu. Lakini hiyo haikuleta tofauti yoyote, kama lilikuwa vazi zuri au la, yeye alitaka kumwona Yesu, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo akalikumbatia hilo pipa la takataka, aweze kulipeleka pale. Kwa hiyo akalipeleka pale mbio, na hapo akawa na takataka mwilini mwote. Vema, haikuleta tofauti yoyote; a—alitaka kumwona Yeye, kwa vyovyote vile.

⁹² Kwa hiyo wakati akilisukuma hilo pipa, huku amelikumbatia, alimsikia mtu fulani akicheka. Naye akaangalia kote, na tazama alikuwa ni Lavinski amesimama pale, mshindani wake, akisema, “Vema, unajua nini! Zakayo ameanza, amepata kazi mpya akiacha mkahawa wake. Anafanya kazi ya kuzoa taka.”

⁹³ Wajua, ibilisi anataka tu kuona kile awezacho kufanya ili kuweka kila kitu njiani mwako, awezacho, kukuzuia kumwona Yesu. Atakuambia, “Hao ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Watakuambia, “Hao ni kundi la wapumbavu.” Atasema, “Hao ni, hawana chochote. Hao ni maskini takataka za jijini,” chochote awezacho kufanya. Lakini kama umekusudia kumwona, Mungu atakutengenezea njia ya kumwona. Liweke tu hilo moyoni mwako. Jambo fulani litatukia, wakati njaa hiyo inapoingia moyoni mwako, kitu fulani. Utaenda kumwona, kwa vyovyote vile.

⁹⁴ Kwa hiyo haikuleta tofauti yoyote. Maskini uso wake ukawa mwekundu, naye aliaibika. Lakini alilisukuma tu hilo pipa, hata hivyo, na akalishika, ndipo akaparamia juu ya mti. Hiyo ni sawa, sivyo, akaparamia? Ninyi watu wa kusini mnajua maana ya *kuparamia*, yaani, akapanda mti, akafika juu ya mti. Basi akafika kule juu, na akapata mahali ambapo matawi mawili yanakutania na kuungana katika shina la mti, na hapo akaketi.

⁹⁵ Sasa, hapo ni mahali pazuri pa kuketi, mahali njia mbili zinapokutana; yako na ya Mungu; wazo lako, na Lake. Huo ni wakati mzuri kuketi na kulitafakari. Mawazo yako mwenyewe kumhusu; na kile Neno Lake lisemacho kwamba Ndiye. Kile unachofikiria kuwa ndicho alichu; na kile Neno lisemacho kwamba ndicho alichu. Kile Ujumbe wa majira ulicho, kwa mawazo yako; na kile Ujumbe wa majira ulicho, kwa Neno Lake. Hiyo ndiyo tofauti. Keti hapo na utafakari huo kwa kitambo kidogo.

⁹⁶ Hapana shaka, Shetani akaja juu ya moja la mabega yake. Akasema, “Unajua nini? Wewe unaonekana wa kupendeza sana, umeketi hapa ukitoa vibanzi kutoka kwa mikono yako. Huku umevalia vazi lako bora kuliko yote, nalo limejaa taka kote. Na sasa jina lako litatangazwa kote jijini, mizaha yote itakuwa juu yako, maana angalia ni kitu cha kijinga jinsi gani ulichofanya, umeketi hapa.”

⁹⁷ Mnaona, Shetani, unapoanza, basi atajaribu kukuambia, “Umekosea.”

⁹⁸ Huyu hapo ameketi, katika hali hiyo! Akasema, “Vema, Rebeka alisema Yeye ni Nabii. Nitampa jaribio. Nitaona kama Yeye ni Nabii.” Sasa akasema, “Atakapokaribia hapa, nitajificha tu, na Yeye hatajua kuwa nipo hapa juu. Kwanza, nitamtazama vizuri. Halafu nikishamwona, basi nitaruka kutoka kwa mti huu, ndipo nitashuka pale chini na nimwambie.” Sasa kasema,

"Sasa, ikiwa Yeye—ikiwa Yeye ni Nabii, hata hivyo, kama Rebeka alivyosema kuwa ndivyo alivyo, huenda akajua kuwa nipo hapa juu kwenye mti huu, ikiwa hiyo ni kweli. Kwa hiyo nakwambia, nitamtia mashakani," kwa hiyo akavuta majani yote karibu naye na kujifunika, kila mahali, hata asingeweza kuonekana; na akaacha jani moja, kuchungulia, wajua, kumwona wakati akipiga kona.

⁹⁹ Ndipo basi akaketi pale, akiliwazia kwa undani. Baada ya kitambo kidogo, alisikia kelele zikikaribia kwenye kona.

¹⁰⁰ Ni ajabu, popote alipo Yeye, daima kuna kelele nyingi. Mnajua, kelele ni dalili ya uhai. Mnaona? Kumbukeni kuhani mkuu, wakati alipovikwa na kuingia katika Patakatifu pa patakatifu, kwenye upindo wa vazi lake alikuwa na komamanga na kengele, na kelele hiyo katika Patakatifu pa patakatifu ilikuwa ndiyo njia ya pekee ambayo wanaongojea walijua kama alikuwa hai au la. Iitoa kelele. Na mahali pasipo na kelele, basi, jamani, huenda amekufa. Vema, nafikiri kwa kiasi kikubwa hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu, leo, hakuna kelele za kutosha kulihusu, hakuna shauku ya kutosha, hakuna kitu cha kutosha. Na kwa hiyo, alipo Yesu, daima kuna kelele.

¹⁰¹ Wakati mmoja, alipoingia Yerusalemu, walikuwa wakipiga mayowe na kupiga makelele, na, "Hosana kwa Mfalme ajaye katika Jina la Bwana!"

¹⁰² Na baadhi ya hao makuhani wakisimama pale, wakasema, "Mbona, wanyamazishe, watulie."

¹⁰³ Akasema, "Wakinyamaza, mawe yatapiga kelele." Kitu fulani hakina budi kusogea akiwepo. Angalia. Na, halafu, wale waliomwamini.

¹⁰⁴ Ndipo basi akasikia kelele hii ikikaribia kwenye kona, na kupiga mayowe na kuendelea. Kwa hiyo akawaza, "Vema, hapana shaka anakaribia." Kwa hiyo akalivuta jani lake, na kuliinua ili kutazama. "Sasa nimempata kabisa. Tutaona Yeye ni Nabii kiasi gani." Kwa hiyo alipokuwa ameketi pale, huku jani lake limeinuliwa, akitazama; na—na juu kwenye mti huu, juu kabisa kupita vichwa vyao, ambapo wangepitia chini ya mti.

¹⁰⁵ Kwa hiyo alipomwona mtu wa kwanza akikaribia kwenye kona, hapana budi alikuwa ni mtume, Petro, maana alikuwa mtu mkubwa, mnene, mwenye nguvu. Ninaweza kumwona akisukuma umati nyuma, akisema, "Marafiki, samahani. Bwana wetu alikuwa na ibada kuu jana usiku, nguvu nyingi zimemtoka. Nyote mtaelewa. Hivi mwaweza kusimama tu kando ili Bwana aweze kupita? Naomba mfanye hivyo." Ndipo hapa akaja Mathayo, Marko, na hao wengine, moja kwa moja, wakisema, "Sasa sisi—sisi hatutaki kuwa jeuri; ha—hatupo hapa kwa kusudi hilo. Lakini Bwana wetu amechoka sana, wala hajapata kiamshakinywa Chake, kwa hiyo tuna—tuna... Tunaomba msimame kando, tafadhali."

¹⁰⁶ Kulikuwa na m—mtu aliyesimama hapo, ambaye labda Zakayo alipata kumtazama.

¹⁰⁷ Siku chache hapo kabla, kwenye mmoja wa mikutano katika mahali pa biashara, da—daktari alikuwa pale, na akamwambia jamaa huyu aliyekuwa na msichana mdogo ambaye alikuwa mgonjwa sana kwa homa, naye asingeendelea kuwa hai ikiwa ninii. . . Alikuwa amefanya yote aliyoweza kwa ajili yake.

¹⁰⁸ Ndipo Zakayo, alipoliinua jani lake, na kutazama, alimwona mtu huyu, akiwa na mtoto huyu amemfunika kwenye blanketi hili, akikaribia kwenye kona. Akawaza, “Ni jambo la kijinga jinsi gani ambalo huyo baba angefanya, kujaribu kumfuata huyo—huyo anayedhaniwa kuwa Nabii! Huyu hapa akaja kwenye kona pamoja na mtoto huyu, na alikuwa na homa, naye amesimama hapa nje kwenye upepo.”

¹⁰⁹ Lakini, mnajua, kama tu vile Zakayo, wakati ukiamini kweli, hakuna kitu kitakachokuzuia, wewe.

¹¹⁰ Naye alitaka kumpeleka huyo mtoto Kwake. Na kila wakati wangepiga ko—kona, ama kugeuka, angesukumwa nyuma. Bali, a—alishikilia, alikuwa anaendelea. Hatimaye, kwenye kona hii, maskini mama huyo akatoka mbio akiwa na mtoto huyo mikononi mwake, na hapana shaka alianguka, ndipo akasema, “Bwana, mrehemu mtoto wangu.” Naye hapo akasimama baba wa mtoto, akilia, pia, ambaye alikuwa ni rafiki yake Zakayo.

Akasema, “Ni kitu gani kilichobadilisha nia yake?”

¹¹¹ Kwa hiyo asingeweza kujua kuwa Mtu huyo ni Nani, bado, Yeye alikuwa kwenye umati. Mara ghafla, anauona mkono ukinyoka na kugusa, juu ya maskini blanketi hili. Ndipo msichana huyo mdogo akafunguliwa, akaenda akirukaruka huko mitaani.

“Sasa lazima kuna jambo kuhusu hilo,” Zakayo akasema.

¹¹² Hatimaye, Yeye aliweza kuonekana. Na kumtazama mara moja tu, Zakayo alikuwa amebadilisha maoni yake. Kumwona tu mara moja! Huyu hapo. Hakuonekana kama mwanadamu. Kulikuwa na kitu tofauti kumhusu Yeye. Mpole, mtulivu, mwenye huruma; na hata hivyo, alionekana kama, iwapo angenena, ulimwengu ungefika mwisho. Alikuwa ni mtu tofauti na kile alichokuwa amewazia. Mtazamo wake ukaanza kuninii. . . Ugumu wake wote ukaanza kutoweka, hapo alipomwona. Anakuja akitembea mtaani. Aliwaza; juu ya jani hili dogo, akitazama huko, kuona kilichokuwa kikiendelea. Na wakati akitembea, alifika moja kwa moja chini ya mahali alipokuwa.

¹¹³ Ndipo akasema, “Unajua, Mtu huyo aweza kuwa ni Nabii. Labda Rebeka alikuwa sahihi. Huenda alijua mengi kuhusu Maandiko kuliko nilivyojua.” Kwa hiyo anatembea moja kwa moja, huku ameinamisha kichwa chake, akiendelea kutembea,

mnyenyekevu, mtulivu, kama alivyofanya daima. Nao wanafunzi wakiwaondoa watu njiani Mwake.

¹¹⁴ Basi alipofika moja kwa moja chini ya mti, alisimama. Zakayo, akitazama juu ya jani, kitu kama *hicho*. Yeye akaangalia juu kwenye mti, kasema, “Zakayo, shuka chini.”

¹¹⁵ Si kwamba tu alijua alikuwa—alikuwa juu kwenye mti, bali alijua jina lake lilikuwa ni Zakayo. Kwa kiwango kikubwa ilikuwa rahisi kwake kushuka kutoka kwenye mti huo, kuliko ilivyokuwa kupanda. Alimjua; muujiza ulifanywa juu yake. Unaona?

¹¹⁶ Akasema, “Bwana, nimekuwa makosani. Niko tayari kukiri kuwa nimekosea. Kama nimechukua kitu, ambacho hakikufaa, ni—nitakilipa. Nitatoa nusu ya mali yangu niwape maskini.”

Yesu akasema, “Leo hii, wokovu umekuja nyumbani mwako.”

¹¹⁷ Ni kitu gani kilichombadilisha? Badiliko lilikuwa ni nini, ndugu na dada? Wazia tu kwa dakika moja. Badiliko lilikuwa kwamba, alikuwa ameona Kitu halisi.

¹¹⁸ Alikuwa amesikia ahadi zote zilizokuwa zimetolewa, kuhani akizungumzia kile *kilichokuwa*, Musa nabii mashuhuri, *hiki* mashuhuri, *kile*, au *kinginecho*, kikiyahidi kitu fulani kikuu katika siku za usoni, huku wakipuza kinachofanywa sasa. Hiyo ndiyo njia ya mwanadamu.

¹¹⁹ Aliona kitu halisi, kitu ambacho angeweza kukiona, mwenyewe. Muujiza ulikuwa umemfanyikia yeye. Huyu alikuwa ni yule Nabii. Kwa sababu, hakumjua, wala asingeweza kumwona juu kwenye mti. Lakini alipofika moja kwa moja chini ya mti, Yeye alisimama na kuangalia juu, na kusema, “Zakayo, shuka chini. Leo, wokovu umekuja nyumbani mwako.”

¹²⁰ Ndugu, ni kitu halisi ndicho hubadilisha moyo wa mtu, hubadilisha fikira zao. Wakati mwingine ni kufinywa, hakika, ili kulifikia. Lakini kama utamjia Kristo, asubuhi ya leo, pamoja—pamoja na wa—wazo moyoni mwako, kwamba, “Sitakuwa mkosoaji, bali nitachunguza Maandiko na kuona kile alichokuwa.”

¹²¹ Kama akija kwenye mkutano, usiku wa leo; kabla hujaja, chunguza uone kile alichokuwa. Chochote kile alichokuwa, hana budi kuwa kitu hicho hicho leo. Ninii Yake . . . Kama nilivyonena jana usiku, kama wengi wenu walikuwepo, mnaona. Je! Mungu hujitambulisha Mwenyewe kwa tabia Yake? Yeye hana budi kubaki hivyo daima, kwa kuwa ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Mioyo ya watu ni—ni ninii sana . . . M—mwanamume au mwanamke anayemcha Mungu kwa kweli, mfanyabiashara, au chochote kile, yeye daima . . . kuna kitu moyoni mwake, iwapo kuna uchaji wowote wa Mungu kwake, kujua kitu kuhusu Mungu.

¹²² Labda, sikuwaambia kilichomfanyikia Zakayo. Alifanyika mshiriki wa tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel, huko Yeriko. Mnaona, ninataka kuwaambieni kumhusu, kwanza, mnaona. Loo, hakika, asingekuwa chochote kingine ila full Gospel, hakika sivyo. Hayo ndiyo yote aliyohubiri Yesu. Kwa hiyo akawa mshiriki hapo. Nawe unapaswa kuwa mshiriki wa lilo hilo. Sasa angalia.

¹²³ Lakini alitaka kuona kitu halisi. Basi alipoona kitu halisi, mwenyewe, kilichothibitishwa Kimaandiko, basi alikuwa tayari. Ni vitu halisi ndivyo huweka mahali pafaapo.

¹²⁴ Hadithi ndogo tu kabla ya kufunga. Ni wangapi humu ndani walio wawindaji, hebu tuone mikono yenu, ndugu zangu humu ndani? Loo, jamani! Ni—nilijua sikuwa peke yangu. Kwa hiyo napenda kuwinda, nami ni . . .

¹²⁵ Nilikuwa nikienda huko juu kwenye misitu ya kaskazini, huko juu New Hampshire. Ni makao ya kulungu mwenye mkia mweupe. Jinsi ninavyopenda kuwawinda! Nami nilikuwa nikienda huko kila mwaka. Na nilikuwa na mshirika huko, jina lake Bert Call, mmoja wa watu wema sana niliopata kuwinda nao.

¹²⁶ Na tabia yangu daima imekuwa ni kupenda mwitu. Nilizaliwa mwituni, na ilionekana tu kana kwamba nililelewa huko. Na hata wongofu wangu haukuuondoa kwangu. Si sana kuwinda wanyama; bali ili tu kuwa mwituni. Nafikiri Mungu yuko huko; kumwona Yeye, jinsi ambavyo Yeye hutembea. Na maumbile, jinsi yanavyokufa na kuingia chini, yakarudi tena, na ufufuo.

¹²⁷ Jua huchomoza asubuhi, mtoto mchanga aliyezaliwa; halafu yapata saa tatu, linaenda shule; na kisha saa nne limekwisha; saa sita liko katika nguvu zake; saa nane alasiri linakaribia umri wangu; halafu saa kumi na moja lina umri wa miaka themanini, linakufa. Linaingia chini. Lilitumikia kusudi la Mungu. Halijafa. Litarudi kesho yake asubuhi. Ni Mungu akishuhudia kuwa kuna uhai, kifo, kuzikwa, kufufuka.

¹²⁸ Iangalie miti huko nje. Majira yaliyopita ya majani kupukutika, utomvu uliingia chini kwenye mzizi kabla ya jalidi ama chochote kingine kuja. Ulikuwa unafanya nini? Kuingia chini kaburini. Kunafanyika nini basi? Unarudi tena kwenye majira ya kuchipua. Haujafa. Huingia chini na kukaa ardhini, unarudi. Ukikaa juu, basi baridi kali itauua. Mnaona? Mungu anayo . . . Hauna akili yake wenyewe ambayo hupeleka huko chini. Ni njia ya Mungu iliyotolewa. Kwa hiyo hufuata tu njia iliyotolewa na Mungu. Huingia chini, hujificha kote kupitia baridi kali, hurudi tena na uhai mpya mwaka ujao, ukishuhudia kuna uhai, kifo, kuzikwa, kufufuka. Kila mahali, ni kitu kile kile; Mungu, katika maumbile Yake makuu, akijishuhudia Mwenyewe.

¹²⁹ Mwindaji huyu, alikuwa ana shabaha sana, hodari wa shabaha. Bali alikuwa ndiye mwanaume katili sana niliyewahi kukutana naye. A—angenidhihaki wakati wote. Aliwapiga risasi watoto wa kulungu.

¹³⁰ Sasa, si makosa kumpiga risasi mtoto wa kulungu kama sheria inasema hivyo. Lakini, mwajua, Ibrahimu alimwua ndama na kumlisha Mungu, kwa hiyo haikuwa ji—jinsia, wala u—ukubwa.

¹³¹ Ni mtazamo. Angewapiga risasi kwa sababu tu ilinichukiza. Naye angesema, “Loo, wewe ni mwoga sana, kama wengine wa hao makuhani.” Kasema, “Billy, ungekuwa mwindaji mzuri kama haikuwa kwamba wewe ni mhubiri.” Tena kasema, “Lakini wewe ni mwoga sana. Hivyo ndivyo walivyo wahubiri,” kasema, “wao ni—wao ni waoga sana.”

Ndipo nikasema, “Bert, wewe ni katili.”

¹³² Alikuwa na macho kama mjesi, hata hivyo. Ndipo akasema... Alifanya, yeye... Kama wanawake wanavyojaribu kupaka rangi macho yao, mnajua, juu namna *hiyo*. Naye akasema... Ndipo akaangalia namna hiyo, na akasema, “Wewe ni mwoga tu.” Kwa hiyo angepiga risasi watoto wa kulungu. Na akiua mmoja, anamwacha hapo, kisha anaenda moja kwa moja kutafuta mwingine, ili tu kunifanya nijisikie vibaya. Ndipo akasema, “Nitakutoa kwa huko kuhubiri, moja ya siku hizi.”

Nami nikasema, “Loo, la, Bert. La, la.”

¹³³ Basi siku moja nilienda huko juu, kwenye majira ya kupukutika, na muda ulikuwa umeenda. Na majira yalikuwa yameingia karibu wiki moja, nami nilikuwa na shughuli nyingi. Nilikuwa Bwana Nyama wa Serikali ya Indiana, na ni—nilikuwa na shughuli nyingi, na moja kwa moja kwenye majira ya kuwinda, kwa hiyo ilinibidi kuchukua likizo yangu. Nilienda huko kwa kuchelewa kidogo.

¹³⁴ Na hao kulungu wenye mkia mweupe, iwapo wametupiwa risasi, unanena kuhusu Houdini kuwa ni bingwa wa kutoweka, jamani, huyo ni mwanafunzi ukilinganisha nao. Na kwa hiyo basi wanajificha kwelikweli. Na ilikuwa ni siku za usiku wa mbalamwezi, theluji ardhini yapata inchi sita, kazi nzuri ya kufuatilia nyayo.

¹³⁵ Na kwa hiyo Bert, alipokuja kwenye kibanda mahali nilipokuwa, akasema, “Niseme, Billy, nina moja kikufaacho mwaka huu.”

Nami nikasema, “Nini?”

¹³⁶ Akatia mkono mfukoni mwake na kukitoa. Alikuwa na filimbi ndogo. Angepuliza, na ilitoa sauti tu kama mtoto wa kulungu anayemlilia mama yake. Mtoto mchanga wa kulungu, mwajua, akimlilia mama yake.

¹³⁷ Nikasema, “Bert, waweza je kuwa katili hivyo?” Nikasema, “Unamaanisha . . . Usingefanya jambo kama hilo!”

Akasema, “Ha-ha, ewe mhubiri mwoga!”

¹³⁸ Ndipo tukaendelea kuwinda, siku hiyo, na tukaenda kwenye Njia nyembamba kwenye mlima wa Jeffersonville. Na haikukupasa kuwa na wasiwasi kumhusu, alijua jinsi ya kuipata njia yake ya kurudi. Kwa hiyo tukapanda juu mpaka yapata adhuhuri, na ndipo tungetengana na kwenda mmoja njia moja, na mmoja njia nyingine. Na halafu tukipata kulungu wetu, tungemning’iniza juu, ha—halafu tungewachukua farasi wetu na kwenda kumleta.

¹³⁹ Kwa hiyo tulifika karibu saa tano, hatukuwa tumeona hata mburuzo, si hata mburuzo mmoja.

¹⁴⁰ Kulungu wote walikuwa wamelala chini. Wangeingia kwenye kichaka, na chini ya lundo la vichaka na kadhalika, ambapo vilele vya miti, ambapo wakata miti walishakuwa. Nao wangeweza, walikuwa wanajificha, wasionekane, maana walikuwa wametupiwa risasi. Waliogopa.

¹⁴¹ Yapata saa tano, Bert akasimama, akaketi. Kulikuwepo mpenyo mdogo yapata, loo, ukubwa wa jengo hili, na nda—ndani yake huenda ikawa ukubwa huu maradufu, mpenyo mdogo pale. Ndipo akaketi chini, kisha akaingiza mkono kutoa, nilidhani, themosi ya—yake aliyokuwa nayo kwenye koti lake. Daima sisi hubeba themosi na kuwa na chokoleti moto, na, maana ina kichochezi ndani yake, mwajua, na—na tunakula sandwichi, na kisha tunatengana. Tulikuwa tunapanda juu kuelekea eneo la miti, kwa hiyo niliwazia kuwa labda Bert alikuwa anaenda kula sandwichi yake. Kwa hiyo aliketi chini kutoa themosi hii na ku . . . nilifikiri alikuwa anaenda kuitoa. Nami nikaacha tu, nikaiweka bunduki yangu chini kuegemea kwenye mti, na nikaanza kuitoa yangu.

¹⁴² Bali, kile alichokuwa, alikuwa akiitoa maskini ile filimbi. Kwa hiyo alipoitoa hii filimbi ndogo, aliipuliza. Na yeyote aliyewahi kumsikia maskini mtoto mchanga wa kulungu akilia, kwa namna fulani ni ya kuchukiza, hata hivyo. Basi alipoipuliza filimbi hiyo, kilichonishangaza, moja kwa moja kando yake, alisimama jike la kulungu mkubwa mnene. Sasa ninii . . . Jike la kulungu ni mama kulungu, mwajua. Kwa hiyo, akasimama. Hayo hapo macho yake makubwa ya hudhurungi, kila moja, kubwa, hayo masikio makubwa yameelekezwa juu namna *hiyo*. Unaona, mtoto wake mchanga alikuwa mashakani.

¹⁴³ Ndipo akaipuliza tena, na huyo kulungu jike akaangalia huku na huku. Na akatembea moja kwa moja kuingia kwenye upenyo huo. Sasa hiyo si kawaida, yeyote wenu wawindaji mnajua hiyo, kwa kulungu kufanya hilo. Akajitokeza pale. Niliweza kuyaona macho yake makubwa. Alikuwa amesimama si zaidi ya yadi ishirini kutoka kwangu. Ndipo nikawaza, “Loo,

Bert, huwezi kufanya hivyo, na kumwua huyo maskini mama wa thamani; huku anamtafuta mtoto wake mchanga, nawe unamhadaa namna hiyo.” Na filimbi hii ilikuwa imelia, naye alikuwa . . . Akajitokeza pale.

¹⁴⁴ Ndipo mwindaji huyo akainua wenzo kwenye bunduki yake ya thelathini-sufuri-sita, akaiangusha chini; hiyo ikaifanya bunduki tayari kufyatua, unajua, huku kinga imeondolewa.

¹⁴⁵ Naye akasikia hiyo. Ndipo akaangalia kote, na akamwona mwindaji huyo. Masikio yake yakainama moja kwa moja. Kwa kawaida walikuwa wameondoka. Na asingekuwa amejitokeza pale, kwa kuanzia, kwenye wakati huo wa siku. Lakini, mnaona, yeye alikuwa mama. Kulikuwa na kitu ndani yake, yeye, kitu halisi, kitu fulani. Hakuwa akiigiza chochote. Alikuwa mama. Alizaliwa mama. Na mtoto wake mchanga alikuwa mashakani, na hiyo ilimjalisha.

¹⁴⁶ Ndipo akaniangalia, na hayo macho yaliyoonekana kama ya mji, na akafinya uso, nikasema, “Bert, usifanye hivyo. Usifanye hivyo.” Akafinya tu uso; akageuka na bunduki hiyo. Loo, jamani!

¹⁴⁷ Alikuwa hodari wa shabaha. Na nilijua kuwa wakati hisia hiyo ya huruma ilipoingia kwenye moyo wake mwaminifu wa mama, angemlipua moja kwa moja. Mnaona? Alisimama umbali usiofika yadi ishirini; risasi kama uyoga, yenye ukubwa wa mia na themanini—kubwa ya mia na themanini, na hapo angaliulipua moyo wake kupitia pande zote.

¹⁴⁸ Nikawazia, “Wawezaje kuwa katili, hata kuulipua moyo wa huyo mama wa thamani, huku yeye anamtafuta mtoto wake mchanga? Wawezaje kufanya hilo, Bert?” Nilikuwa nikijiwazia. Nikaona mikono yake ikiimarika. Nisingeweza kutazama hilo. Nisingeweza kabisa kulitazama. Nikageuza mgongo wangu. Ni—nisingeona hilo.

¹⁴⁹ Mama huyo wa kweli na mtiifu amesimama pale. Hakuwa mnafiki. Hakuwa tu akiigiza hilo, kwa onyesho. Alikuwa mama. Hiyo ndiyo sababu alikuwa akifanya hilo. Kifo hakikumaanisha chochote kwake. Mtoto wake mchanga alikuwa mashakani. Aliwaza zaidi kumhusu mtoto wake kuliko alivyowaza kuhusu maisha yake mwenyewe. Acha wawindaji wapige risasi chochote kile; moyo wake mtiifu ulikuwa ukidunda, umama wake. Umama ndani yake ulikuwa ukiita. Mtoto wake mchanga alikuwa analia. Kulikuwa na kitu ndani yake, kilicho halisi, kilikuwa kinadunda.

¹⁵⁰ Na ingewezekanaje huyo mwindaji katili kuulipua huo moyo mtiifu? Nisingeangalia hiyo. Nikageuza kichwa changu. Nikawaza, “Bwana Mungu, usimwache afanye hivyo.” Nilikuwa nimesimama *hivi*, nisingeweza kusikia . . . sikutaka kuisikia bunduki hiyo ikifyatuka. Hilo lilivuka mpaka. Nikangojea.

¹⁵¹ Bunduki hiyo haikufyatuka. Ndipo nikageuka na kuangalia, nayo ilikuwa ikienda namna *hii*. Asingeweza kuifyatua.

¹⁵² Aligeuka na kuniangalia, nayo hayo macho makubwa yalikuwa yamegeuka. Machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake. Aliniangalia, huku midomo yake ikitetemeka. Akaitupa bunduki hiyo kwenye lundo la theluji, kisha akanishika kwenye mguu wa suruali. Akasema, “Billy, nimepata ya kutosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake.”

¹⁵³ Hapo kwenye hilo lundo la theluji, nilimwongoza kwa Bwana Yesu. Kwa nini? Aliona kitu halisi. (Alishakuwa katika aina zote za makanisa.) Aliona kitu fulani ambacho hakikuwa ni maigizo. Aliona kitu ambacho ni cha kweli.

¹⁵⁴ Enyi marafiki, huenda tukawa na kanuni za kanisa na masharti ya kanisa, na theolojia na kila kitu kingine, bali kuna Yesu halisi wa kweli. Hebu tumtazamie Yeye hivi sasa huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa maombi.

¹⁵⁵ Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ningependa kuwaulizeni swali; mियो yenu imeinamishwa, pia. Ni wangapi humu ndani sasa, ninyi mnaoukiri Ukristo, ambao hamuukiri, ikiwa maungamo ndiyo yote mliyo nayo? Lakini ni wangapi wenu wangetaka kuwa Wakristo kadiri yule kulungu alivyokuwa mama, na kitu cha halisi sana ndani yako, kinachoonekana kuwa ni zaidi ya maisha yako ama chochote ulicho nacho? Nawe unasema, huenda ukasema hili, “Ndugu Branham, mimi ni mshiriki wa kanisa. Mimi ni mwanamume mfanyabiashara, mwanamke mfanyabiashara, ama chochote kingine, mke nyumbani. Bali, kweli, kuwa Mkristo wa jinsi hiyo, hata ningeweza kuweka ulimwengu wote kando, nivumilie kukosolewa au chochote kile; ni—ningetaka kuwa hivyo, ningetaka kuwa Mkristo moyoni mwangu, kama yule kulungu alivyokuwa mama.”

¹⁵⁶ Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, na macho yenu yamefumbwa. Mbele za Mungu, nawaulizeni, katika Jina la Kristo, kwenye mwisho wa wakati, hivi waweza tu kuinua mkono wako? Siwezi kufanya wito wa madhabahuni, maana hapana nafasi. Lakini wewe sema tu, “Niombe, Ndugu Branham, kwamba niwe namna ya Mkristo kama yule kulungu alivyokuwa mama.” Mungu awabariki. Ipo tu mikono kila mahali. “Hebu niwe Mkristo kiasi hicho.”

¹⁵⁷ Sasa, Zakayo, unapoinua mkono wako, hiyo inaonyesha kuwa Yeye amekupata. Sasa mbona usishuke upesi kutoka mtini? Ataenda nyumbani pamoja nawe leo hii kwa mlo wa kutwa. Atakaa nawe siku zote za maisha yako.

¹⁵⁸ Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya Bwana Yesu, Uwepo Wake. Nasi tunafahamu kwamba kuna kitu hapa kilichowafanya wanaume na wanawake... Baadhi yao hata wamekiri kuwa Wakristo, kwa miaka. Bali kulikuwa, kuna kitu

Fulani hapa kilichowafanya; hata ingawa wameungama, kama vile Zakayo alikuwa, bali wakati mguso wa Kristo, wameinua mkono wao kama ushuhuda kwamba kitu Fulani ndani yao kiliwaambia wafanye hivyo. Jalia wajue sasa hivi kwamba huyo ni Yesu. Alikuwa apitie njia hii, asubuhi ya leo, Naye amepita.

¹⁵⁹ Kulikuwapo, nadhani, mikono mia moja na hamsini iliyoinuliwa, Bwana. Naomba ya kwamba Wewe utamtembelea kila mmoja, na kuwapa uhalisia wa kuwa Mkristo halisi. Na haijalishi ni kiasi gani ulimwengu unajaribu kutuvunja moyo, na ni kiasi gani wengine wanavyojaribu kutuvunja moyo, jalia tujue ya kwamba ni vita kufika Kule. Ni jitihada inayotubidi kufanya. Bali tukiunganishwa na Kitu kilicho halisi, cha kweli, Hicho hutubadilisha basi. Ninaomba ya kwamba Wewe utaubadilisha kila moyo, Bwana, na kumfanya kila mtu katika Uwepo wa Kiungu, wakati huu. Mweke Roho Mtakatifu maishani mwao, kuwa Mkristo kiasi kama yule mama kulungu alivyokuwa mama. Alizaliwa mama. Na jalia wazaliwe kwa Roho wa Mungu, na kuwa mfuasi halisi wa Yesu Kristo. Jalia washuke kutoka kwenye miti yao ya mkuyu leo hii. Tujalie, Bwana. Naomba uende nyumbani na kila mmoja wetu, na hapo ukae nasi hadi wakati utakapokuja kutupeleka kwenye Makao yetu ya Milele. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁶⁰ Asanteni, sana. Bwana awabariki. Nimewachelewesha. Nilipaswa kuwa nimetoka hapa saa nne. Ni saa tano kasoro dakika kumi.

¹⁶¹ Natumaini kwamba Mungu atachukua maneno haya machache yasiyo ya kistadi, na ya harakaharaka na wasiwasi, na kuyalishia miyoni mwenu. Kumbukeni, kuna kitu halisi kumhusu Kristo. Mungu awabariki. Vema.



ILIMPASA KUPITIA NJIA HII SWA64-0321B

(He Was To Pass This Way)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 21 Machi, 1964, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Kimataifa cha Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Supper Club kule Baton Rouge, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org